Kukumbuka, Kutafakari na Kujenga Upya:

Mwaka Mmoja Tangu Matukio ya **29 Oktoba 2025**



“Kuwakumbuka waliopoteza maisha, kutafakari mafunzo yaliyopatikana, kutathmini changamoto za sasa na maendeleo yaliyofikiwa, na kuweka dira ya taifa salama zaidi, lenye ustahimilivu na umoja wa kudum”.



1.0 UTANGULIZI NA KUMBUKUMBU YA MATUKIO YA 29 OKTOBA 2025

Leo ni mwaka mmoja tangu kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa tarehe 29 Oktoba 2025 na kutokea kwa matukio ya vurugu, matumizi ya nguvu, vifo, majeruhi, kupotea kwa watu na uharibifu wa mali wakati na baada ya uchaguzi huo. Katika kumbukumbu hii, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unaungana na familia zilizofiwa, majeruhi, watu wanaotafuta wapendwa wao, watoto waliopoteza wazazi au walezi wao, wafanyabiashara na wananchi wote walioathirika. Kila maisha yaliyopotea yalikuwa na thamani isiyoweza kupimwa kwa takwimu pekee. Tofauti za kisiasa, hali ya kijamii au tuhuma za kutenda kosa adhabu yake sio kifo na haindoi wajibu wa Serikali na vyombo vya dola wa kulinda uhai wa wananchi.

Tunatumia siku hii kukukumbuka matukio hayo na wote waliopoteza maisha kwa kuwasha mshumaa, kufanya maombi na kutafakari ni kwa jinsi gani kama taifa tumelichukulia swala hili mwaka mmoja sasa. Tutanafanya tathmini yah atua zilizochukuliwa na namna jinsi Taifa ilivyofanyia kazi mapendekezo mbalimbali. THRDC inatafakari siku hii kwa kuwaleta baadhi ya wananchama wake na wadau wake.

Kumbukumbu hii inajengwa juu ya hotuba ya Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Kuchunguza Matukio ya Ghasia na Uvunjifu wa Amani Yaliyotokea Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, alipowasilisha ripoti ya Tume tarehe 23 Aprili 2026. Aidha, kumbukumbu hii inazingatia mapendekezo, nyaraka zilizowahi kutolewa na THRDC pamoja na asasi zingine za kiraia kwa serikali, taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa, vyama vya siasa ikiwemo Chama cha Mapinduzi kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025. Nyaraka hizo na mapendekezo hayo yalikuwa yanahimiza mazungumzo ya kitaifa, maboresho ya sheria za uchaguzi, kulindwa kwa uhuru wa kiraia, kushughulikiwa kwa matukio ya utekaji na kupotea kwa watu, na kuhuishwa kwa mchakato shirikishi wa Katiba Mpya.

1.1 Historia na Muktadha wa Matukio ya Uchaguzi Mkuu wa 29 Oktoba 2025

Matukio ya Oktoba 2025 hayawezi kutazamwa bila kuzingatia mazingira ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yaliyotangulia kabla ya uchaguzi. Katika hotuba yake ya tarehe 23 Aprili 2026, Jaji Chande alieleza kwamba Tume ilipokea maeneo 31 yaliyotajwa na mashahidi kuwa chanzo cha ghasia, kisha ikabainisha vyanzo vitano na vichocheo nane. Vyanzo



hivyo vilihusu, miongoni mwa mambo mengine, madai ya Katiba Mpya, changamoto za demokrasia ya vyama vingi na mfumo wa uchaguzi, ugumu wa maisha na ukosefu wa ajira, malalamiko kuhusu rushwa na utekaji au kupotea kwa watu, changamoto za utendaji wa taasisi za umma na masuala ya uhusiano wa kimataifa.

Kabla ya uchaguzi, THRDC pamoja na asasi nyingine za kiraia ziliwasilisha mapendekezo yaliyosisitiza umuhimu wa mazungumzo ya kitaifa, mabadiliko ya sheria na mifumo ya uchaguzi, uhuru wa kiraia, kushughulikia matukio ya utekaji na upotezwaji wa watu na kuhuisha mchakato jumuishi wa Katiba Mpya. Miongoni mwa nyaraka hizo ni waraka wa pamoja wa asasi za kiraia wenye kichwa ***"Hali ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Muafaka wa Kitaifa",*** uliowasilishwa kwa Chama Cha Mapinduzi kupitia THRDC tarehe 22 Oktoba 2025. Kuwepo kwa mapendekezo hayo kabla ya uchaguzi kunaonesha umuhimu wa kushughulikia malalamiko na tahadhari mapema, kwa njia ya mazungumzo na utawala wa sheria.

Tume ya Jaji Chande ilifanya uchunguzi katika maeneo 202 yaliyokuwa yameathirika zaidi, katika wilaya 21 za mikoa 11, na kutembelea pia maeneo ya sampuli yasiyokuwa na ghasia. Ilisikiliza waathirika 1,323, kuchukua maelezo ya kiapo kutoka kwa waathirika 953, kupokea madodoso 4,891 na kutumia taarifa za kitabibu, picha na ushahidi mwingine wa kitaalamu.

1.2 Takwimu za Vifo, Majeruhi, Watu Waliopotea na Uharibifu wa Mali za Umma na Binafsi

THRDC inawakumbuka kwa heshima watu wote waliopoteza maisha, bila kujali itikadi, hadhi, umri au mahali walipotokea. Tunatambua majonzi ya wazazi waliopoteza watoto, watoto waliopoteza wazazi au walezi, wenza waliopoteza wapendwa wao, na familia ambazo hadi sasa zinatafuta majibu kuhusu ndugu zao. Tunatambua pia madhara ya majeraha ya kudumu, msongo wa mawazo, kupotea kwa kipato na kusimama kwa shughuli za kiuchumi. Kumbukumbu ya kitaifa ina maana pale inapolinda hadhi ya waliofariki, kusikiliza waathirika na kutafuta njia za kurejesha haki.

a) Vifo

Pamoja na kwamba kumekuwa na mvutano kuhusu idadi halisi ya watu walipoteza maisha, walau takwimu rasmi hadi sasa ni zile ambazo tumetolewa na Tume ya Jaji Chande.Kwa mujibu wa hotuba ya Jaji Chande ya tarehe 23 Aprili 2026, Tume ilibaini vifo 518 vilivyotokana na ghasia za uchaguzi: wanaume 490 na wanawake 28. Kati ya waliofariki, 21 walikuwa watoto; raia walikuwa 502 na maafisa au askari wa vyombo vya ulinzi na usalama 16. Mikoa iliyotajwa kuwa na vifo vingi zaidi ni Dar es Salaam

(182), Mwanza (90), Mbeya (80) na Arusha (53). Kati ya vifo 518, watu 373 walifikishwa hospitalini wakiwa wamefariki, 121 walifariki walipokuwa wakipatiwa matibabu, na kwa vifo 24 hakukuwa na taarifa kutoka vituo vya afya..

b) Uchunguzi wa vifo na miili

Tume ilieleza kuwa uchunguzi wa maiti ulifanyika kwa miili 260 na uchunguzi wa vinasaba kwa miili 274. Katika uchambuzi wa kitaalamu wa taarifa za uchunguzi wa maiti 219, vifo 197 vilihusishwa na kupigwa risasi na 22 havikuhusishwa na risasi. Tume pia ilitaja miili tisa ambayo haikutambuliwa na haikuchukuliwa; sita ilikuwa imezikwa na mitatu ilikuwa Hospitali ya Taifa Muhimbili hadi tarehe 31 Machi 2026. Hata hivyo, wananchi wamekuwa na maoni tofauti kuhusu idadi halisi ya watu waliouwawa wakidai kuwa watu waliouwawa ni wengi zaidi kwasababu hata Tume yenyewe haikufika maeneo yote nchini kwahiyo takwimu hizi sio timilifu.

Tume ilikiri kwamba idadi ya vifo inaweza kubadilika kutokana na uwezekano wa kuwepo kwa familia zilizozika miili bila kuifikisha katika vituo vya afya au majeruhi waliotibiwa nje ya mfumo rasmi na baadaye kufariki. Aidha, ilipokea ushahidi kuhusu watu 39 waliodaiwa kupotea, wakiwemo waliodaiwa kuonekana katika vituo vya afya kabla ya miili yao kutopatikana tena.

c) Hoja ya wananchi kuhusu ukamilifu wa takwimu

Pamoja na umuhimu wa kazi ya Tume, baadhi ya wananchi na familia za waathirika wameeleza mashaka kuhusu iwapo idadi ya vifo 518 inaakisi kikamilifu madhara yaliyotokea. Mashaka hayo yanapaswa kuangaliwa kwa kuzingatia tahadhari iliyotolewa na Tume yenyewe. Katika hotuba ya tarehe 23 Aprili 2026, Jaji Chande alieleza uwezekano wa kuwepo kwa familia zilizozika wapendwa wao bila kufikisha miili katika vituo vya afya au bila kupata nafasi ya kutoa ushahidi mbele ya Tume, pamoja na majeruhi waliotibiwa nje ya mfumo rasmi na kufariki bila taarifa zao kufikishwa kwenye mamlaka husika. Kwa maneno ya Tume yenyewe, ***“idadi ya vifo iliyotolewa kwenye Ripoti hii inaweza isiwe ya mwisho (not final and conclusive)***.

d) Majeruhi

Hadi tarehe 31 Machi 2026, Tume ilitaja majeruhi 2,390 waliopata huduma katika vituo vya afya vya umma na binafsi, wakiwemo raia 2,270 na maafisa au askari wa vyombo vya ulinzi na usalama 120. Kati yao, majeruhi 219 walikuwa na majeraha makubwa, ambapo 197 walikuwa na majeraha yaliyotokana na risasi; majeruhi 2,171 walitajwa kuwa na majeraha madogo.



e) Watu waliopotea

Hotuba ya Jaji Chande ilinukuu takwimu za Jeshi la Polisi kwamba, katika kipindi cha 2023–2025, watu 758 waliripotiwa kupotea, kutekwa au kujiteka; watu 513 walipatikana na 245 hawakuwa wamepatikana, huku mashauri manane yakifunguliwa na upelelezi ukiendelea.

f) Uharibifu wa mali

Kwa mujibu wa hotuba ya Tume, thamani ya mali zilizoharibiwa ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 125, zikiwemo shilingi bilioni 89 za mali za sekta binafsi (asilimia 71.2) na shilingi bilioni 36 za mali za umma (asilimia 28.8). Mali za umma zilizotajwa zilihusisha mali za taasisi za Serikali na huduma za umma, ikiwemo shule, TRA, Mahakama, Polisi, DART, TANROADS, TANESCO na TTCL. Uharibifu huo uliathiri pia shughuli za biashara, ajira, usafiri na huduma muhimu kwa wananchi.

Katika mkutano na wahariri tarehe 25 Novemba 2025, Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba alitaja magari binafsi 1,642, vituo vya mafuta 672 na pikipiki za bodaboda 2,268 kuwa ni mali zilizoathirika.

1.3 Haki ya Kuishi, Utu wa Binadamu na Wajibu wa Dola wa Kulinda Uhai na Mali

Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inalinda haki ya kuishi; Ibara za 12 na 13 zinahusu utu na usawa wa binadamu mbele ya sheria. Ibara za 18, 20 na 21 zinahusu, kwa mtiririko huo, uhuru wa maoni na kutoa taarifa, uhuru wa kukusanyika na kujumuika, na ushiriki wa wananchi katika shughuli za utawala wa nchi. Haki hizi zinafungamana na wajibu wa dola wa kuhakikisha usalama wa watu na mazingira ambayo raia wanaweza kushiriki katika masuala ya umma bila hofu.

Kimataifa, Ibara ya 6 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) inalinda haki ya kuishi, na Ibara ya 21 inalinda uhuru wa kukusanyika kwa amani. Ibara ya 4 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu inalinda haki ya uhai na utu. Uwepo wa maandamano, vitendo vya uhalifu au uharibifu wa mali hauondoi wajibu wa vyombo vya dola kuheshimu haki za watu ikiwemo haki ya kuishi, nguvu inapaswa kutumika kwa mujibu wa sheria na kwa uwiano.

Hotuba ya Jaji Chande ilieleza kuwa Tume ilipokea madai ya watu kupigwa risasi, kujeruhiwa au kuuawa hata katika maeneo ambayo hayakuwa na vurugu au maandamano, ikiwemo ndani ya nyumba na maduka. Tume ilieleza kuwa madai hayo ni mazito na yanahitaji upelelezi wa kina wa kijinai.

Mkataba wa Minnesota wa mwaka 2016 kuhusu Uchunguzi wa Vifo Vinavyoweza Kuwa Kinyume cha Sheria (Minnesota Protocol on the Investigation of Potentially Unlawful Death) unatoa mwongozo wa uchunguzi wa haraka, huru, wa kina na wenye uwazi. Wajibu wa kulinda uhai unaenda sambamba na kulinda mali za umma na binafsi na kuhakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya wahusika wa uharibifu, bila kutumia uharibifu huo kama sababu ya kupuuza haki za binadamu.

1.4 Umuhimu wa Kumbukumbu, Ukweli, Haki na Uwajibikaji katika Kujenga Amani ya Kudumu

Mwaka mmoja baada ya matukio ya Oktoba 2025, kumbukumbu hii si tukio la kuangalia yaliyopita pekee. Ni nafasi ya kitaifa ya kutafakari thamani ya uhai, kutambua maumivu ya waathirika, kutafuta ukweli na kuimarisha imani ya wananchi katika utawala wa sheria. Katika hotuba yake, Jaji Chande alieleza umuhimu wa ***"kutibu majeraha, kuwajibika kila panapostahili",*** akisisitiza pia kujifunza kutokana na yaliyotokea. THRDC inaamini kwamba maridhiano yenye maana yanahitaji ukweli unaoaminika, ushiriki wa waathirika, haki, uwajibikaji na hatua za kuzuia ukiukwaji wa haki kujirudia. ***Waswahili Husema ,Taifa lisilokumbuka misiba yake ni Taifa lisilo kumbuka furaha zake.***

Miongoni mwa mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume tarehe 23 Aprili 2026 ni Serikali kutenga siku ya maombolezo ya kitaifa; kutoa matibabu na huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii; kupata Katiba Mpya ifikapo mwaka 2028; kuunda Tume ya Maridhiano na Muafaka wa Kitaifa; na kufanya uchunguzi wa kijinai kuhusu matukio tatanishi ya vifo, majeruhi na miili ambayo haijapatikana.

Katika kujenga kumbukizi yenye maana, uponyaji wa kitaifa na maridhiano ya kweli, tunakumbushwa na mafundisho ya dini zote mbili kwamba haki, rehema, msamaha, amani na ulinzi wa uhai ni misingi muhimu ya jamii yenye mshikamano. Qur'an inatufundisha kuwa ***"Waumini ni ndugu; basi patanisheni kati ya ndugu zenu" (Qur'an 49:10),*** jambo linalosisitiza wajibu wa kujenga maridhiano na kurejesha mahusiano yaliyovunjika. Aidha, ***Qur'an 41:34*** inatukumbusha kujibu uovu kwa namna iliyo bora zaidi ili uhasama uweze kubadilishwa kuwa ukaribu. ***Qur'an 42:40*** inaunganisha haki na msamaha, huku ikitoa nafasi kwa maridhiano na kurekebisha madhara yaliyotokea. Vilevile, ***Qur'an 2:178–179*** inasisitiza thamani ya uhai, haki na uwajibikaji, na kutukumbusha kwamba kulinda maisha na kuzuia madhara ni msingi wa jamii yenye amani.



Kwa upande wa Biblia pia inaunganisha haki, amani na uponyaji. ***Wakolosai 3:13–15*** vinahimiza kuondoa uchungu, hasira na uadui na badala yake kujenga huruma, msamaha, upendo na amani. ***2 Wakorintho 5:18–19*** inaeleza maridhiano kama jukumu muhimu la kurejesha mahusiano yaliyovunjika, huku ***Mithali 15:1*** ikikumbusha kwamba jibu la upole linaweza kupunguza hasira na kuzuia migogoro kuongezeka. Kwa maana hiyo kutenga tarehe 29 kuwa siku ya kumbukizi ya 29 Ocober ni kujibu uovu kwa upole na kubadili uhasama kuwa mshikamano. ***"Those who cannot remember the past are condemned to repeat it. (Wasioweza kukumbuka historia wapo katika hatari ya kuridia historia) - George Santayana, 1905***

Mafundisho haya yanaendana moja kwa moja msisitizo wetu kuwa na kumbukizi ya kitaifa haitalenga maombolezo pekee, bali pia ***kutafuta ukweli, kutenda haki, kuwaenzi wahanga, kuponya majeraha, kujenga upya uaminifu na kuhakikisha matukio kama hayo hayajirudii tena.*** Kwa msingi huo, kumbukizi inaweza kuwa jukwaa la kitaifa la kuunganisha jamii, kuimarisha mshikamano na kujenga utamaduni wa haki, amani na maridhiano.

2.0 TATHMINI YA TAARIFA NA MAPENDEKEZO YA TAASISI NA WADAU KUHUSU MATUKIO YA 29 OKTOBA 2025

2.1 Utangulizi

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025, taasisi za Umoja wa Mataifa, mashirika ya kimataifa na kikanda, waangalizi wa uchaguzi, asasi za kiraia, vyama vya kitaaluma, vyama vya siasa, viongozi wa dini na wananchi walieleza mitazamo kuhusu vifo, majeruhi, matumizi ya nguvu, uhuru wa kiraia, uharibifu wa mali, mchakato wa uchaguzi na hitaji la maridhiano ya kweli ya kitaifa. Sehemu hii inarejea taarifa mbalimbali zilizotolewa na taasisi hizo na wadau pamoja na mapendekezo yao ili kuonyesha yaliyosemwa kabla, wakati na baada ya matukio hayo.
Maeneo yanayojitokeza katika taarifa nyingi ni umuhimu wa kulinda uhai yaani haki ya kuishi , uchunguzi huru na wa kina, uwajibikaji wa kisheria, haki za waathirika, kuheshimu uhuru wa kujieleza na kukusanyika, mazungumzo jumuishi, Katiba Mpya na mabadiliko ya mifumo ya uchaguzi na taasisi za haki jinai.

2.2 Taasisi za Kimataifa

(a) Umoja wa Mataifa na Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu (OHCHR)

Tarehe 31 Oktoba 2025, msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Stéphane Dujarric, alieleza wasiwasi kuhusu vifo na majeruhi baada ya uchaguzi na kuitaka Serikali kufanya uchunguzi huru na usio na upendeleo kuhusu madai ya matumizi ya nguvu kupita kiasi. Pia alisisitiza umuhimu wa kuheshimu haki za kukusanyika kwa amani, kujieleza na kupata taarifa, pamoja na kuhimiza mazungumzo jumuishi. Kwa upande wake, msemaji wa Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu (OHCHR), Seif Magango, alieleza wasiwasi kuhusu taarifa za mauaji, majeruhi na matumizi ya silaha wakati wa maandamano. Alisisitiza kuwa matumizi ya nguvu yanapaswa kuzingatia misingi ya ulazima na uwiano kwa mujibu wa viwango vya haki za binadamu.



(b) Umoja wa Ulaya (EU)

Katika tamko lililotolewa na Baraza la Umoja wa Ulaya tarehe 2 Novemba 2025, EU ilieleza wasiwasi kuhusu vurugu, kuzimwa kwa intaneti, taarifa za dosari za uchaguzi, vifo na majeruhi. Ilihimiza mamlaka kujizuia kutumia nguvu, kuachia wanasiasa wanaoshikiliwa na kuhakikisha haki za waliofikishwa mahakamani, kuchunguza kwa haraka madai ya utekaji na upotezwaji, na kufanya mazungumzo ya wazi na jumuishi kwa ajili ya maridhiano ya kweli ya kitaifa.

2.3 Taasisi za Kikanda

(a) Umoja wa Afrika (AU)

Tarehe 5 Novemba 2025, Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Afrika, ulioongozwa na Rais Mstaafu wa Botswana Mokgweetsi Masisi, ulisema kuwa uchaguzi wa 2025 haukukidhi viwango husika vya AU na vya kimataifa vya uchaguzi wa kidemokrasia. Ujumbe ulitaja changamoto za mazingira ya kisiasa, kuzimwa kwa intaneti, madai ya matumizi ya nguvu kupita kiasi, na hitaji la mabadiliko ya kikatiba na kisiasa. Uliomboleza vifo na uharibifu wa mali na kuhimiza uchunguzi wa uwazi na haki kwa waathirika.

(b) Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

Tarehe 3 Novemba 2025, Ujumbe rasmi wa Waangalizi wa Uchaguzi wa SADC ukiongozwa na Richard Msowoya, uliwasilisha taarifa ya awali kuhusu uchaguzi wa Tanzania. Ujumbe ulieleza kwamba uchaguzi haukukidhi kikamilifu matakwa ya Kanuni na Miongozo ya SADC kuhusu Uchaguzi wa Kidemokrasia. Ulipendekeza mapitio jumuishi ya Katiba na sheria za uchaguzi, kuimarisha uhuru na uwazi wa taasisi za uchaguzi na kutatua migogoro kwa njia za amani.

(c) Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

Tarehe 5 Novemba 2025, Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ukiongozwa na Dkt. Speciosa Wandira Kazibwe, ulieleza kwamba vurugu katika baadhi ya maeneo ziliathiri shughuli za uangalizi wa upigaji na uhesabuji wa kura. Ulipendekeza kuimarisha elimu ya uraia na mpiga kura, matumizi ya teknolojia, uwazi wa usimamizi wa uchaguzi, uzingatiaji wa maadili ya uchaguzi na utatuzi wa migogoro kwa amani.

(d) Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR)

Katika tamko lililochapishwa tarehe 1 Novemba 2025, Tume ilieleza wasiwasi kuhusu kuzimwa kwa intaneti wakati wa uchaguzi na kusisitiza haki ya kupata taarifa na uhuru wa kujieleza. Tume ilieleza wasiwasi kuhusu taarifa za vifo, majeruhi na matumizi ya nguvu wakati wa vurugu za uchaguzi. Ilihimiza mamlaka kuzingatia ulazima na uwiano katika matumizi ya nguvu, kuchunguza madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu, kuhakikisha uwajibikaji na kutoa haki kwa waathirika. Pia ilihimiza Tanzania kuridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora.

2.4 Taasisi za Umma na Mashirika ya Ndani

(a) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan

Katika hotuba yake ya tarehe 23 Aprili 2026, alipokuwa akipokea ripoti ya Tume ya Jaji Chande, Rais Samia Suluhu Hassan alieleza masikitiko kuhusu matukio ya Oktoba 2025 akisema: “Leo kungekuwa na uwezekano, tunatamani siku zirudi nyuma, yaliyotokea Oktoba 2025 yawe hayakutokea, na historia ijiandike upya ili tuweze kufuta doa tuliloingia.” Aidha, alieleza hatua zinazokusudiwa na Serikali, zikiwemo uchunguzi wa kina, kuundwa kwa Tume ya Maridhiano, hatua za mchakato wa Katiba, na msaada wa matibabu kwa majeruhi.

(b) Tume ya Rais ya Kuchunguza Matukio ya Ghasia na Uvunjifu wa Amani (Tume ya Jaji Chande)

Pamoja na kwamba hadi sasa hakuna taarifa kamili kwa umma, katika hotuba ya tarehe 23 Aprili 2026, Mwenyekiti wa Tume, Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, aliwasilisha matokeo ya uchunguzi kuhusu matukio ya uchaguzi. Tume ilitaja vifo 518, majeruhi 2,390 na uharibifu wa mali wenye thamani ya takribani shilingi bilioni 125. Tume ilieleza pia kwamba takwimu za vifo zinaweza zisiwe za mwisho kwa sababu haikuwafikia waathirika wote. Katika mapendekezo ya muda mfupi, ilitaka matibabu ya bure kwa majeruhi waliopata ulemavu, siku ya maombolezo ya kitaifa, msaada wa kisaikolojia, Katiba Mpya ifikapo 2028, Tume ya Maridhiano na Muafaka wa Kitaifa, utekelezaji kamili wa sheria ya INEC, na uchunguzi wa kijinai wa matukio tatanishi ya vifo, watu zaidi ya 700 waliotekwa, majeruhi na miili ambayo haijapatikana.

Kwa mujibu wa taarifa ya Tume, kati ya vifo 518 vilivyobainishwa, wanaume walikuwa 490 na wanawake 28; watoto walikuwa 21, wakiwemo wawili wenye umri wa chini ya miaka mitano. Tume ilieleza kuwa idadi hiyo huenda isiwe ya mwisho kutokana na kutowafikia waathirika wote na uwezekano wa baadhi ya vifo kutorekodiwa katika vituo vya afya. Aidha, Tume ilipokea taarifa kuhusu watu 39 waliodaiwa kutoweka.



Kuhusu majeruhi, Tume iliripoti watu 2,390 waliopata matibabu hadi tarehe 31 Machi 2026, wakiwemo raia 2,270 na maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama 120. Kati yao, 219 walikuwa na majeraha makubwa, na 197 kati ya hao walikuwa na majeraha yaliyotokana na risasi. Tume ilitambua kwamba takwimu za vituo vya afya vilivyofikiwa huenda hazikujumuisha kila aliyejeruhiwa. Ilipendekeza matibabu ya bure kwa majeruhi waliopata ulemavu mkubwa, pamoja na huduma za ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia kwa waathirika na familia zao.

Kuhusu mali, Tume ilikadiria uharibifu wa takribani shilingi bilioni 125, zikiwemo shilingi bilioni 89 za mali binafsi na shilingi bilioni 36 za mali za umma. Mali zilizoathirika zilijumuisha biashara, maduka, vituo vya mafuta, magari na miundombinu ya huduma za umma. Uharibifu huo uliathiri mitaji, kipato na ajira za baadhi ya wananchi na wafanyabiashara. Taarifa hizi zinaonesha umuhimu wa kutambua waathirika na kuthibitisha hasara zao kabla ya maamuzi kuhusu msaada au fidia.

(c) Asasi za kiraia na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)

Tarehe 4 Novemba 2025, THRDC na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) walitoa tamko la pamoja kuhusu taarifa za vifo, majeruhi, ukamataji na watu wasiojulikana walipo baada ya uchaguzi. Walilaani matumizi ya nguvu kupita kiasi dhidi ya raia na uharibifu wa mali, walitaka kusitishwa kwa ukamataji holela, kulindwa kwa haki ya maandamano ya amani, serikali kutoa taarifa ya watu waliokuwa hawajulikani walipo na kutolewa kwa msaada wa kisheria kwa waathirika ikiwemo watu wote waliokamatwa. THRDC ilipendekeza Octoba 29 kila mwaka kuwa siku ya kumbukizi ya matukio na mauaji ya wakati na baada ya uchaguzi.

THRDC na TLS walieleza pia athari za kuzimwa kwa intaneti kwa mawasiliano na shughuli za uchumi. Tarehe 7 Novemba 2025, LHRC, Twaweza, Foundation for Civil Society, JamiiAfrica na zingine walitoa tamko la pamoja wakieleza wasiwasi kuhusu mauaji yanayodaiwa, utekaji, ukamataji, vizuizi vya habari na kukatika kwa intaneti. Walipendekeza uchunguzi huru na wa wazi, uwajibikaji, haki kwa familia, fidia, uhuru wa kujieleza na mazungumzo jumuishi.

2.5 Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa vilitoa misimamo tofauti kuhusu uchaguzi na matukio yaliyofuata. Tarehe 4 Mei 2026, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Kenani Kihongosi, alieleza utayari wa chama kushirikiana katika utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Jaji Chande, yakiwemo maridhiano na hatua za kikatiba.

CHADEMA, ambayo haikushiriki uchaguzi, ilipinga mwenendo na matokeo yake. Katika msimamo uliowasilishwa tarehe 11 Desemba 2025 na John Heche Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, chama kilitaka uchunguzi huru wa kimataifa kuhusu vifo na madai ya ukiukwaji wa haki, fidia kwa waathirika, Katiba Mpya na mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi.

ACT-Wazalendo ilieleza kutoridhishwa na mwenendo wa uchaguzi; katika taarifa ya 10 Aprili 2026 kuhusu mazungumzo na mjumbe wa Jumuiya ya Madola, chama kilitaka uchunguzi huru, mazungumzo jumuishi, uwajibikaji na mabadiliko ya Katiba na mfumo wa uchaguzi.

2.6 Taasisi na Vyama vya Kitaaluma

(a) Chama cha WanasheriaTanganyika (TLS)
Tarehe 4 Novemba 2025, TLS na THRDC walilaani taarifa za vifo, majeruhi, ukamataji na matumizi ya nguvu dhidi ya raia kufuatia uchaguzi. Rais wa TLS, Wakili Boniface Mwabukusi, alisisitiza umuhimu wa kulinda haki za msingi, kutoa msaada wa kisheria kwa waathirika na kufanya uchunguzi unaoaminika. Tarehe 7 Novemba 2025, Mwabukusi alipinga matumizi ya mashtaka ya uhaini dhidi ya baadhi ya waliokamatwa kufuatia maandamano na kuhimiza uchunguzi huru. TLS pia ilishiriki katika hatua za msaada wa kisheria na kufungua shauri la kikatiba kuhusu amri ya kutotoka nje iliyotolewa na IGP wakati wa uchaguzi.

2.7 Wananchi na Familia za Waathirika

Wananchi na familia za waathirika walieleza haja ya kufahamu ukweli kuhusu ndugu zao waliopoteza maisha au wasiojulikana walipo, kupokea miili kwa mazishi yenye heshima, na kupata uchunguzi huru na unaoaminika. Walisisitiza pia umuhimu wa kusikilizwa kwa sauti za waathirika na kushirikishwa katika hatua za kutafuta haki.

Familia ziliomba matibabu endelevu kwa majeruhi, msaada wa kisaikolojia na kijamii, msaada wa kisheria, na ulinzi wa watoto waliopoteza wazazi au walezi. Wananchi na wafanyabiashara walioathiriwa na uharibifu wa mali walisisitiza umuhimu wa utaratibu wa wazi wa kutathmini hasara na kupata msaada au fidia stahiki. Kwa jumla, mapendekezo yao yalijikita katika ukweli, utu, haki, uwajibikaji na hatua za kuzuia madhara hayo kujirudia.



2.8 Taasisi za Kidini na Viongozi wa Imani

(a) Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC)

Tarehe 15 Novemba 2025, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), kupitia Rais wake Askofu Wolfgang Pisa, lilitoa tafakari ya pamoja kuhusu yaliyotokea siku na baada ya Uchaguzi Mkuu wa 29 Oktoba 2025, kufuatia mkutano wa maaskofu wa tarehe 11–14 Novemba 2025. Walipendekeza uchunguzi huru na wa kuaminika unaoshirikisha wadau wa ndani na nje, uwajibikaji wa viongozi wenye dhamana, huduma za kitabibu kwa majeruhi, kushughulikia miili ya waliopoteza maisha, kuachiwa kwa waliokamatwa katika mazingira ya matukio hayo, kuanzishwa upya kwa mchakato wa Katiba Mpya na kusikilizwa kwa malalamiko ya wananchi. TEC ilisisitiza kuwa haki na ukweli ni msingi wa maridhiano ya kudumu.

(b) Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT)

Katika taarifa iliyoripotiwa tarehe 14 Novemba 2025 na vyombo vya habari, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Askofu Dkt. Stanley Hotay, aliunga mkono wito wa maridhiano ya kitaifa baada ya Uchaguzi Mkuu wa 29 Oktoba 2025. CCT ilipendekeza mazungumzo jumuishi yanayowashirikisha wadau wote ili kutafakari yaliyotokea, kushughulikia tofauti na kuimarisha amani, umoja na haki. Pia iliiomba Serikali kutoa msaada wa kibinadamu kwa familia zilizoathirika, kuwasaidia majeruhi na kurejesha utulivu. CCT ilisisitiza kuwa amani ya kweli inahitaji haki kutendeka.

(c) Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA)

Tarehe 14 Novemba 2025, vyombo vya habari viliripoti tamko la Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na taasisi washirika, lililosomwa na Sheikh Issa Othman, mjumbe wa Baraza la Ulamaa. BAKWATA ilieleza kusikitishwa na vifo, majeruhi na uharibifu wa mali uliofuatia uchaguzi, lakini ilihusisha chanzo cha vurugu na vitendo vya uhalifu, uporaji na uharibifu wa miundombinu. Iliitaka Serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini waliochochea, kupanga na kuongoza vitendo hivyo na kuchukua hatua dhidi ya wahusika. Ilisisitiza umuhimu wa amani inayozingatia haki.

Aidha, tarehe 21 Novemba 2025, viongozi wa taasisi za Kiislamu, wakiwemo wa BAKWATA, waliwasilisha mpango wa hoja 17 wa kuimarisha amani na maridhiano. Akizungumza kwa niaba ya taasisi hizo, Sheikh Mussa Kundecha aliunga mkono kuundwa kwa tume ya uchunguzi na mazungumzo ya kitaifa; alitaka uchunguzi wa kina usio na upendeleo, kuwawajibisha wenye hatia bila kuwaonea wasio na hatia, kusaidia familia zilizopoteza ndugu au mali na kushughulikia sababu za msingi za vurugu.

2.9 Tathmini ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Taasisi na Wadau Mbalimbali Nchini

2.9.1 Utangulizi

Tathmini iliyofanywa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) inaonyesha kuwa kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025, taasisi, asasi za kiraia na wadau mbalimbali walitoa mapendekezo yaliyolenga kuimarisha demokrasia, utawala wa sheria, ulinzi wa haki za binadamu, uwajibikaji na maridhiano ya kitaifa. Baadhi ya mapendekezo hayo yalitolewa kabla ya uchaguzi, siku ya uchaguzi na baada ya uchaguzi kwa lengo la kuzuia migogoro ya kisiasa na ukiukwaji wa haki za binadamu. Mapendekezo yaliyotolewa baada ya uchaguzi, yalilenga kushughulikia madhara ya matukio hayo na kuzuia kujirudia kwake.

Tathmini ya THRDC inabainisha kuwa, hadi 29 Oktoba 2026, baadhi ya hatua zimechukuliwa, baadhi zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, huku mapendekezo mengine mengi na muhimu yaliyotolewa na wadau mbalimbami ikiwemo ya Jaji Chande Tume ya yakiwa bado hayajatekelezwa.

2.9.2 Mapendekezo Yaliyotekelezwa

Serikali ilichukua hatua ya kuunda Tume ya Rais ya Kuchunguza Matukio ya Ghasia na Uvunjifu wa Amani yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025. Tume hiyo, iliyoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, iliwasilisha matokeo na mapendekezo yake tarehe 23 Aprili 2026. Hatua hii ilijibu kwa sehemu wito wa wadau waliotaka uchunguzi wa matukio hayo, ingawa haikukidhi kikamilifu madai ya baadhi ya wadau waliopendekeza uchunguzi huru wenye ushiriki wa kimataifa. Muundo wa Tume ulilalamikiwa kwa sehemu kubwa na wadau na wananchi.

2.9.3 Mapendekezo Yaliyotekelezwa kwa Sehemu au Yenye Hatua Zinazoendelea

Kuhusu uchunguzi na uwajibikaji, Serikali ilichukua hatua ya kuunda Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Wahusika wa Ghasia na Ukiukwaji wa Sheria katika matukio yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025. Tume hiyo ilizinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 7 Agosti 2026, kufuatia mapendekezo ya Tume ya Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman.

Tume hiyo ina wajumbe sita, wakiongozwa na Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania, Shaaban Ali Lila, pamoja na majaji kutoka Tanzania, Uganda na Namibia.



Wajumbe wa kimataifa ni Jaji Petrus Tileinge Damaseb, Naibu Jaji Mkuu wa Namibia, na Jaji Barishaki Bonny Cheborion wa Mahakama ya Rufani ya Uganda na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki. Tume ilipewa muda wa miezi mitano kuchunguza wahusika wa ghasia, matumizi ya nguvu, vifo, majeruhi na upotezwaji wa watu, na kuwasilisha ripoti pamoja na mapendekezo ya hatua za kisheria na kiutawala. Tume hiyo inaendelea na uchunguzi hadi sasa na pia wadau wengi na wananchi pia wameendelea kukosoa Tume hii pamoja na muundo wake na wengine kuona hakukuwa na ulazima wa tume hii badala yake tungekuwa na Tume Huru ya Uchunguzi.

2.9.4 Mapendekezo Ambayo Utekelezaji Wake Haukufanyika, Haujaanza au Kuwekwa Wazi kwa Umma

(a) **Katiba Mpya:** Pendekezo la kuhuisha mchakato jumuishi wa Katiba Mpya, lililotolewa na THRDC, asasi za kiraia, wananchi , vyama vya siasa na Tume ya Jaji Chande, bado halijaonesha hatua za utekelezaji zenye ratiba rasmi na ushiriki mpana wa wananchi.

(b) **Maridhiano ya kitaifa:** Pendekezo la kuanzisha mazungumzo jumuishi na kuunda Tume ya Maridhiano na Muafaka wa Kitaifa halijaonesha utekelezaji wa mfumo rasmi unaoshirikisha vyama vyote vya siasa, asasi za kiraia, viongozi wa dini na makundi mengine ya wananchi.

(c) **Mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi:** Mapendekezo ya AU, SADC, EAC na wadau wengine kuhusu kuimarisha uhuru wa taasisi za uchaguzi, uwazi, ushindani wa kisiasa na haki za wapiga kura hayajaonesha utekelezaji kamili.

(d) **Uchunguzi wa utekaji na upotezwaji wa watu:** Pendekezo la kuunda Tume huru kuchunguza matukio ya utekaji ya miaka mitano iliyotangulia uchaguzi halijatekelezwa. Zaidi ya watu 700 wanarepotiwa kupotea na kutekwa. Baadala yake matukio ya utekaji yameendelea kushamiri zaidi.

(e) **Kupatikana kwa watu wasiojulikana walipo:** Hakuna taarifa kamili iliyowekwa wazi kwa umma kuhusu hatima ya watu wote walioripotiwa kupotea wakati wa matukio ya onctober 29, ikiwemo wale waliotajwa katika ushahidi uliopokelewa na Tume ya Jaji Chande.

(f) **Uwajibikaji kwa vifo na matumizi ya nguvu:** Hakuna afisa yeyote wa Serikali aliyewajibika au kuwajibishwa kutokana na mauaji yaliyotokea Oktoba 29, 2025.

(g) **Uchunguzi huru wenye ushiriki wa kimataifa:** Pendekezo kuhusu uchunguzi huru wa kimataifa halijatekelezwa kikamilifu; ushiriki wa majaji kutoka Uganda na Namibia katika Tume Jaji Lila ulikosolewa na kuonyesha kuwa haiwezi kuwa mbadala wa Tume Huru ya Kimataifa ambayo imekuwa ikipendekezwa.

(h) **Fidia kwa familia za waliopoteza maisha:** Utekelezaji wa utaratibu wa fidia au msaada wa kifedha kwa familia zote za waliopoteza maisha haujatekelezwa

(i) **Matibabu ya bure kwa majeruhi:** Pendekezo la Tume ya Jaji Chande la kuwapatia matibabu ya bure majeruhi waliopata ulemavu mkubwa halijathibitishwa kutekelezwa kikamilifu kwa walengwa wote.

(j) **Huduma za kisaikolojia na kijamii:** Hakuna taarifa kamili iliyowekwa wazi kuhusu mpango wa kitaifa wa kuwapatia huduma za ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia waathirika na familia zao.

(k) **Msaada kwa watoto waliopoteza wazazi au walezi:** Hakuna taarifa kamili ya Serikali kwa umma kuhusu utaratibu mahsusi wa kuhakikisha watoto walioathirika wanapata malezi, elimu, ulinzi na msaada wa kijamii.

(l) **Fidia kwa uharibifu wa mali:** Utekelezaji wa utaratibu wa kuthibitisha hasara na kutoa fidia au msaada kwa wananchi na wafanyabiashara walioharibiwa mali haujawekwa wazi kikamilifu.

(m) **Siku ya maombolezo ya kitaifa:** Pendekezo la THRDC na Tume ya Jaji Chande la kutenga siku ya maombolezo ya kitaifa kwa ajili ya waliopoteza maisha halijawekwa wazi au kutekelezwa kikamilifu

(n) **Haki za waliokamatwa na kushitakiwa:** Hakuna taarifa jumuishi iliyowekwa wazi kuhusu hatima ya watu wote waliokamatwa kutokana na matukio ya uchaguzi, isipokuwa wachache waliachiwa na wengine kufungwa katika mahakama mbalimbali nchini.

(o) **Uhuru wa kujieleza na kukusanyika:** Mapendekezo kuhusu kulinda haki ya maandamano ya amani, uhuru wa kujieleza na kuzuia matumizi ya nguvu kupita kiasi hayajaonesha utekelezaji kamili wa hatua za kiutendaji zilizochukuliwa na Serikali.

(p) **Uhuru wa habari na upatikanaji wa intaneti:** Hakuna taarifa ya kutosha kuhusu hatua mahsusi za kuhakikisha huduma za intaneti hazizimwi kiholela na vyombo vya habari vinaweza kuripoti matukio ya uchaguzi bila vizuizi visivyo halali na Serikali haijawahi kueleza sababu za kuzima intaneti wakati wa uchaguzi.



(q) **Uwajibikaji wa vyombo vya ulinzi na usalama:** Mapendekezo kuhusu kuboresha utendaji wa vyombo vya usalama, kuimarisha uhusiano na wananchi na kuzuia matumizi ya nguvu yasiyo ya lazima bado hayajaonesha matokeo kamili yanayoweza kupimwa kwasababu kuna matukio kadhaa yameendelea kuripotiwa kuhusu ukamataji unaotumia nguvu.

(r) **Mabadiliko ya taasisi za haki jinai:** Mapendekezo ya kuboresha mifumo ya uchunguzi wa makosa, ukamataji, upelelezi na uwajibikaji wa taasisi za haki jinai hayajatekelezwa

(s) **Ushiriki wa wananchi na vijana:** Mapendekezo ya Tume ya Jaji Chande kuhusu kuimarisha ushiriki wa vijana na kuanzisha Baraza la Taifa la Vijana hayajaonesha utekelezaji kamili unaoweza kuthibitishwa.

(t) **Kuridhiwa kwa Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora:** Pendekezo la ACHPR la Tanzania kuridhia mkataba huo halijatekelezwa

(u) **Kuundwa kwa Baraza la Ushauri la Wazee:** Pendekezo la Tume ya Jaji Chande la kuanzisha Baraza la Ushauri la Wazee kwa ajili ya kusaidia juhudi za maridhiano, mshikamano na utatuzi wa migogoro ya kitaifa halijatekelzwa

(v) **Kuridhiwa kwa mikataba ya kimataifa kuhusu utekaji na mateso:** Pendekezo la THRDC na asasi za kiraia la Tanzania kusaini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Watu Wote Dhidi ya Kupotezwa kwa Kulazimishwa na Mkataba dhidi ya Mateso halijatekelezwa

(w) **Kuanzishwa kwa chombo huru cha kushughulikia malalamiko dhidi ya vyombo vya usalama:** Pendekezo la kuwepo kwa taasisi huru yenye mamlaka ya kupokea, kuchunguza na kufuatilia malalamiko dhidi ya vyombo vya usalama halijaonesha utekelezaji wa mfumo wenye uhuru na uwajibikaji unaoweza kuthibitishwa.

UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO 22 YA TUME YA JAJI CHANDE OTHMAN

Hali ya utekelezaji hadi 29 Oktoba 2026 | Chanzo: Hotuba ya 23 Aprili 2026 na Tathmini ya THRDC ya Oktoba 2026

Na.	Pendekezo	Hali ya utekelezaji
1	Matibabu ya bure, vifaa saidizi na viungo bandia kwa majeruhi waliopata ulemavu.	Haijathibitishwa utekelezaji wake hadi sasa
2	Kutenga siku ya Maombolezo ya Kitaifa kuwakumbuka waliofariki.	Hadi sasa Haijatekelezwa
3	Mkakati, rasilimali na tathmini ya haraka ya huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii.	Haijathibitishwa utekelezaji wake hadi sasa
4	Kuunda Kamati ya Wataalamu wa Katiba na kupata Katiba Mpya itakayopigiwa kura ya maoni.	Hadi sasa Haijatekelezwa
5	Kuunda Tume shirikishi ya Maridhiano na Muafaka wa Kitaifa.	Hadi sasa Haijatekelezwa
6	Kuunda Baraza la Wazee la Ushauri kwa ajili ya kusaidia maridhiano.	Hadi sasa Haijatekelezwa
7	Kutekeleza kikamilifu sheria ya INEC, uteuzi wa viongozi na kuipa uwezo wa kuajiri watumishi hadi jimboni.	Hadi sasa Haijatekelezwa
8	Kuunda Tume maalumu ya uchunguzi wa kijinai kuhusu wahusika wakuu, vifo, majeruhi na miili isiyopatikana.	Tume imeundwa -Utekelezaji unaendelea
9	Jeshi la Polisi kubuni na kutekeleza mkakati wa kurejesha uhusiano wake na jamii.	Haijathibitishwa utekelezaji wake hadi sasa
10	Serikali na vyombo vya dola kuheshimu ushindani wa vyama vingi vya siasa.	Utekelezaji wake bado una changamoto ,baadhi ya vyama vya siasa vinapitia wakati mgumu
11	Kusimamia maadili ya viongozi na kudhibiti rushwa, ufisadi na mienendo isiyofaa.	Utekelezaji haujawekwa wazi
12	Kutekeleza Sheria ya Baraza la Taifa la Vijana na kuanzisha Baraza.	Hadi sasa Haijatekelezwa
13	Kuimarisha uwajibikaji wa watendaji, utatuzi wa kero, na vitengo vya ufuatiliaji na tathmini.	Hadi sasa Haijatekelezwa- Kero zilizopolekea maandamano bado hazijaanza fanyiwa kazi
14	Kuweka kipaumbele katika kutekeleza mapendekezo ya Tume zilizopita, ikiwemo Tume ya Haki Jinai.	Hadi sasa Haijatekelezwa, utekelzaji wa mapendekezo ya tume ya Jaji Chande ya Haki jinai unaendelea kutekelezwa
15	Kuimarisha uteuzi na ajira kwa sifa na ushindani wa haki, na kutenganisha utumishi na ushawishi wa kisiasa.	Hadi sasa Haijatekelezwa
16	Kuimarisha usalama, ulinzi na ufuatiliaji wa mipaka	Utekelezaji unaendelea
17	Kuimarisha ulinzi shirikishi na kurejesha mfumo wa nyumba kumi kisheria.	Haijathibitishwa utekelezaji wake hadi sasa
18	Kusimamia kwa uwazi mikopo, ajira, zabuni na fursa za miradi kwa vijana.	Utekelezaji haujawekwa wazi
19	Kupitia bajeti, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuelekeza fedha kwenye uwezeshaji kiuchumi.	Hadi sasa Haijatekelezwa
20	Kupanua Sheria ya Usimamizi wa Maafa kujumuisha uvunjifu wa amani, mawasiliano na mazoezi ya dharura.	Utekelezaji haijawekwa wazi
21	Kurejesha mafunzo ya lazima ya JKT kwa wahitimu wote wa kidato cha sita na kuwasaidia kujiajiri.	Utekelezaji unaendelea
22	Kubuni na kutekeleza mkakati wa makazi maalumu kwa vyombo vya ulinzi na usalama.	Utekelezaji haujawekwa wazi



3.0 WITO NA MAPENDEKEZO YA THRDC

Kwa kuzingatia mwaka mmoja tangu matukio ya tarehe 29 Oktoba 2025, tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu, pamoja na matokeo ya Tume ya Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unatoa wito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taasisi za umma na wadau wengine kuchukua hatua zifuatazo ili kuhakikisha ukweli, haki, uwajibikaji, maridhiano na kuzuia matukio kama hayo kujirudia.

(a) Kutangaza tarehe 29 Oktoba kuwa Siku ya Kitaifa ya Kumbukumbu na Tafakari: Serikali itangaze rasmi tarehe 29 Oktoba ya kila mwaka kuwa siku ya kuwakumbuka na kuwaenzi wote waliopoteza maisha katika matukio ya Uchaguzi Mkuu wa 2025, bila ubaguzi. Siku hiyo iwe fursa ya kitaifa ya kuomboleza, kutafakari thamani ya uhai, kuenzi waathirika na kujenga dhamira ya pamoja ya kuzuia matukio kama hayo kujirudia.

(b) Kuharakisha mchakato jumuishi wa Katiba Mpya: Serikali ianzishe na kuweka wazi ratiba ya kuhuisha mchakato wa Katiba Mpya, kwa kushirikisha wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar, vyama vya siasa, asasi za kiraia na wadau wengine. Mchakato huo uzingatie mapendekezo yaliyotolewa kabla ya uchaguzi pamoja na pendekezo la Tume ya Jaji Chande la kupatikana kwa Katiba Mpya ifikapo mwaka 2028, kabla ya chaguzi za mwaka 2029 na 2030.

(c) Kuanzisha maridhiano ya kweli na muafaka wa kitaifa: Serikali ianzishe Tume au utaratibu huru na jumuishi wa maridhiano ya kitaifa, itakayoweka ukweli wa matukio , kuweka uwajibikaji na wenye hadidu za rejea zinakubalika na umma, ratiba na uongozi unaokubalika. Maridhiano yashirikishe vyama vya siasa, familia za waathirika, vijana, wanawake, viongozi wa dini, asasi za kiraia na wananchi kwa ujumla, bila kuwa mbadala wa uchunguzi wa kijinai na uwajibikaji wa kisheria.

(d) Kuweka wazi Ripoti ya Tume ya Jaji Chande: THRDC inamuomba Rais kuruhusu kuchapishwa kwa ripoti kamili ya Tume ya Jaji Chande ili wananchi, familia za waathirika na taasisi husika waweze kufahamu matokeo, ushahidi na mapendekezo ya Tume. Serikali pia iweke wazi hatua zinazochukuliwa kutekeleza mapendekezo hayo.

(e) **Kuhakikisha uchunguzi huru, ukweli na uwajibikaji:** Taifa liihakikishe uchunguzi wa kina, huru na usio na upendeleo kuhusu vifo, majeruhi, watu waliopotea na madai ya matumizi ya nguvu kinyume cha sheria. Uchunguzi ubaini waliohusika moja kwa moja na waliotoa amri, uhifadhi ushahidi na kuwezesha hatua za kisheria kwa kuzingatia Itifaki ya Minnesota ya mwaka 2016 na haki za wote wanaohusika.

(f) **Kutoa matibabu na msaada wa kijamii kwa waathirika:** Serikali ianzishe utaratibu maalumu wa kuwapatia majeruhi matibabu endelevu bila malipo, vifaa saidizi, huduma za afya ya akili, ushauri nasaha na msaada wa kisheria. Watoto waliopoteza wazazi au walezi na familia zilizoathirika wapatiwe msaada unaozingatia mahitaji yao ya maisha, malezi na elimu.

(g) **Kuweka utaratibu wa fidia na urejeshaji wa haki:** Serikali iandae mfumo wa wazi, wa haki na unaofikika wa kuthibitisha madhara na kutoa fidia stahiki kwa familia za waliopoteza maisha, majeruhi na wananchi walioathiriwa na uharibifu wa mali. Utaratibu huo uzingatie pia athari za kiuchumi, kupotea kwa kipato na mahitaji ya muda mrefu ya waathirika.

(h) **Kufanya mabadiliko katika Jeshi la Polisi na taasisi za haki jinai:** Serikali itekeleze mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai ya mwaka 2023 na ya Tume ya Jaji Chande, hususan kuhusu weledi, uwajibikaji, matumizi halali ya nguvu, uhusiano kati ya Polisi na jamii na ulinzi wa mikusanyiko ya amani. Aidha, iimarishe mfumo huru wa kushughulikia malalamiko dhidi ya vyombo vya usalama.

(i) **Kukomesha utekaji na upotezwaji wa watu:** Serikali iunde chumbo huru cha kijaji kichunguze kwa kina matukio yote ya utekaji na upotezwaji wa watu yaliyotokea kabla, wakati na baada ya uchaguzi, na kuhakikisha familia zinapatiwa taarifa kuhusu hatima ya ndugu zao. Aidha, Tanzania izingatie kusaini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Watu Wote Dhidi ya Kupotezwa kwa Kulazimishwa na Mkataba dhidi ya Mateso, pamoja na kuimarisha ulinzi wa mashahidi na waathirika.

(j) **Kuimarisha uhuru wa kiraia na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu:** Serikali ihakikishe uhuru wa kujieleza, kukusanyika kwa amani, kupata taarifa na kufanya shughuli halali za kisiasa na kiraia unalindwa kwa vitendo. Hatua zichukuliwe kuzuia ukamataji holela, vitisho na matumizi yasiyo halali ya nguvu dhidi ya wananchi, waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu na viongozi wa kisiasa, pamoja na kuhakikisha huduma za intaneti hazizuiliwi kinyume cha sheria.



(k) **Kufanya mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi:** Serikali, Bunge na taasisi zinazohusika zifanyie kazi mapendekezo ya waangalizi wa uchaguzi wa Umoja wa Afrika, SADC, EAC na wadau wa ndani kuhusu uwazi, usawa wa ushindani wa kisiasa, uhuru wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na uaminifu wa mchakato wa uchaguzi. Mabadiliko hayo yafanyike kwa ushirikishwaji mpana ili kurejesha imani ya wananchi katika taasisi na michakato ya kidemokrasia.

(l) **Kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo unakuwa wazi na unaopimika:** Serikali iweke wazi mpango wa utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Jaji Chande na taasisi nyingine, ukibainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa, taasisi zinazowajibika, muda wa utekelezaji na matokeo yaliyofikiwa. Taarifa za maendeleo zitolewe kwa umma mara kwa mara ili wananchi waweze kufuatilia utekelezaji na kupima uwajibikaji wa Serikali.

4.0 HITIMISHO

THRDC inaamini uongozi wenye maono huacha urithi si kwa kufuta kumbukumbu za nyakati ngumu, bali kwa kuzikabili kwa ujasiri, kuzitafakari kwa hekima, na kuzitumia kujenga taifa lenye umoja, haki na maridhiano ya kudumu. Kwa maana hiyo, THRDC inatoa wito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulipokea na kulifanyia tathimini na mapendekezo ya THRDC kuhusu Matukio ya Oktoba 2025. Utekelezaji wa mapendekezo haya isiwe njia ya kufufua chuki au kuongeza migawanyiko, bali iwe nafasi ya kuenzi maisha, kutafuta ukweli, kutenda haki, kujenga maridhiano na kuchukua hatua zinazopimika kuhakikisha matukio kama hayo hayajirudii. ***António Guterres: "Remembering the past is crucial to safeguarding the future." "Kukumbuka yaliyopita ni muhimu katika kuulinda mustakabali."***

"TUNAWAKUMBUKA WAHANGA, TUNAJIFUNZA KUTOKANA NA HISTORIA, NA TUNACHUKUA HATUA KUHAKIKISHA YASIJIRUDIE TENA." (NEVER AGAIN)

Mratibu Wa Kitaifa -THRDC- 29/10/2026

Wakili Onesmo Olengurumwa

Taifa linalosahau Misiba yake haliwezi kumbuka furaha yake



Mikocheni B, Eyasi Road, P.O.Box 105926,
Dar Es Salaam, Tanzania

+255 769 642208

info@thrdc.or.tz

www.thrdc.or.tz

Tufuatilie kwenye mitandao ya kijamii

Tanzania Human Rights
Defenders Coalition

@thrdcoalition

@thrdcoalition